Tanzania Human Rights Defenders Coalition
[THRDC]
P. O. Box 105926 Dar es Salaam, Tanzania
Mob: +255 769 642 208 E-mail; info@thrdc.or.tz
Website: www.thrdc.or.tz

# TAMKO KUHUSU USHIRIKI WA ASASI ZA KIRAIA KATIKA UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA

## Introduction

Sisi wanachama wa Mtandao wa Watetezi wa haki za binadamu Tanzania (THRDC), tunaoshiriki katika mkutano mkuu wa mwaka wa wanachama, tumesikitishwa na hali ya ushiriki mdogo wa Asasi za Kiraia (AZAKI) katika mchakato mzima wa uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajiwa kufanyika Tarehe 24 Novemba 2019. Kutokana na changamoto mbalimbali, zikiwemo kucheleweshwa au kukosekana kwa vibali vya ushiriki wa AZAKI katika kutoa elimu ya uraia kwa wapiga kura na uangalizi wa uchaguzi, ushiriki wa AZAKI umeshuhudiwa kuwa ni mdogo sana.

## Changamoto za Ushiriki wa AZAKI katika Uchaguzi

Katika kipindi cha miezi kadhaa sasa Mtandao umeshuhudia changamoto mbalimbali zinazoathiri nafasi ya Watetezi wa Haki za Binadamu/AZAKI katika nchi yetu wakati wa uchaguzi na michakato mingine ya kidemikrasia. Baadhi ya changamoto hizo ni pamoja na:

i. Mtazamo hasi wa umma juu ya kazi za Watetezi wa Haki za Binadamu ambayo inahusishwa, pamoja na mambo mengine, ufahamu mdogo wa haki za Watetezi wa Haki za Binadamu nchini Tanzania;
ii. Watetezi wa Haki za Binadamu kupewa majina mbalimbali yanayoharibu taswira yao kwa mfano kuitwa Wanasiasa. Hii pia imechangiwa na vitendo vya baadhi ya Watetezi wa Haki za Binadamu, aidha kwa kujua ama bila kujua kwa kushiriki katika shughuli za moja kwa moja za kisiasa kama vile kufanya kampeni katika uchaguzi na kugombea nafasi za kisiasa wakati bado wanashikilia nafasi zao za uongozi katika AZAKI;
iii. Baadhi ya Viongozi wa Serikali kushindwa kuchora mstari wa kutofautisha kati ya shughuli za kisiasa zinazokatazwa kisheria na shughuli zingine halali zinazotekelezwa na AZAKI bila kuunga mkono chama chochote cha siasa
iv. Ugumu wa kupata idhini ya mamlaka husika kwa ajili ya kutoa elimu ya uraia kwa wapiga kura, ufuatiliaji na uangalizi wa uchaguzi; na,
v. Kucheleweshwa kwa vibali na wengine kutokupewa barua rasmi ya majibu kuhusu maombi ya kushiriki katika kutoa elimu ya uraia au
vi. Kukosekana kwa fedha za kutosha kwa ajili ya utekelezaji wa kazi mbalimbali wakati wa uchaguzi.

Kwa miaka kadhaa hatukuwa na kanuni rasmi ambazo zingeweza kutoa mwongozo juu ya namna wanachama wa THRDC na Watetezi wa Haki za Binadamu wanaweza kufanya kazi kwa ufanisi na bila kupendelea chama chochote katika uchaguzi na michakato mengine ya kidemokrasia nchini Tanzania. Hii imesababisha uwepo wa malalamiko dhidi ya Watetezi wa Haki za Binadamu kuwa wamekuwa wakijihusisha na shughuli za moja kwa moja za kisiasa. Katika miaka michache iliyopita, Mtandao ulitambua uwepo wa changamoto hiyo na kupitia

Board of Directors:
Ms. Vicky Ntetema, Michael Kyande, Kenneth Simbaya, Deogratius Nsokolo, Maxence Melo, Christina Kamili, Jamila M. Juma, Hassan Kh. Juma, Edwin Soko.
*Defending Human Rights is not a Crime!*

Mpango Mkakati wake mpya wa mwaka (2018-2022), Mtandao uliamua kuunda kanuni rasmi ambazo zitatumika kama mwongozo kwa Watetetezi wa Haki za Binadamu wakati wanajihusisha na kazi mbalimbali  wakati wa uchaguzi na michakato mingine ya kidemokrasia.

Isitoshe, imebainika kuwa wakati wa chaguzi zilizopita, Watetezi wa Haki za Binadamu walikabiliwa na matukio mengi ya usalama kama vile, mashambulio, kukamatwa, kutekwa nyara, vitisho na matukio mengine kama hayo. Ili kuzuia changamoto kama hizi, Mtandao umeamua kuandaa kanuni hizi ili ziwe mwongozo kwa wanachama wa THRDC na Watetezi wa Haki za Binadamu katika shughuli hizo.

Miaka ya 2019 na 2020 ni miaka maalum kwa demokrasia ya nchi yetu. Hii ni kwa sababu chaguzi kuu mbili zinatarajiwa kufanywa ndani ya kipindi hiki. Mwisho wa mwaka 2019 taifa letu litakuwa likiendesha Uchaguzi wake wa Serikali za Mitaa ambao baadaye utafuatiwa na Uchaguzi Mkuu mnamo 2020. Chaguzi hizi zinakuja kufuatia uchaguzi mkuu wa mwaka 2015 ambao uliiweka madarakani serikali ya awamu ya 5 chini ya Rais John Pombe Magufuli.

Tunapoelekea kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa mnamo Novemba 24, 2019 na uchaguzi mkuu mwaka 2020, Mtandao umeshuhudia ongezeko kubwa la changamoto zinazoathiri utendaji kazi wa Watatetezi wa Haki za Binadamu / AZAKI zinapojaribu kufanya shughuli zao za kawaida katika uchaguzi. Baadhi ya changamoto hizo ni pamoja na ugumu na taratibu ngumu kwa Watetezi wa Haki za Binadamu / AZAKI kupata idhini kutoka kwa mamlaka husika kwa ajili ya kutoa elimu ya uraia kwa wapigakura, ufuatiliaji na uangalizi wa uchaguzi.

Kwa mujibu wa utafiti mdogo ambao umefanywa na Mtandao, kati ya AZAKi 86 ambazo zilihojiwa, mashirika kumi na nane (18) yaliomba idhini kutoka kwa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ili kutoa elimu ya uraia kwa wapiga kura. Kati ya mashirika hayo 18 ni mashirika manne (4) tu yameruhusiwa kutoa elimu ya uraia kwa wapigakura

Utafiti pia umeonyesha kuwa kati ya AZAKI 86 zilizofikiwa katika utafiti huo, AZAKI 14 ziliomba idhini ya ufuatiliaji na uangalizi wa uchunguzi. Kati ya hizo, ni mbili tu (2) ambao wameidhinishwa kufuatilia na kuangalia uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka huu.

Changamoto nyingine ya ushiriki wa AZAKI katika uchaguzi imekuwa ukosefu wa fedha za kutosha kuziwezesha kushiriki kikamilifu kwa kufanya shughuli zinazohitajika. Kati ya mashirika 86 ambayo yamefikiwa na utafiti huo, ni mashirika manne tu (4) wamepata fedha kutoka kwa washirika kwa ajili ya utoaji wa elimu ya uraia kwa wapiga kura na ni 6 tu ndio yamepata fedha kwa ajili ya kufuatilia na kuangalia uchaguzi wa serikali za mitaa.

Walakini, licha ya changamoto zote hizo AZAKI kadhaa zimeendelea kufanya kazi mbalimbali wakati wa uchakuzi kupitia mitandao mbalimbali ya AZAKI. Kati ya AZAKI 86 zilizofikiwa katika utafiti, zaidi ya AZAKI 50 zimejihusisha na shughuli za uchaguzi kwa kufanya kazi kupitia mitandao yao ya AZAKI.

Pamoja na changamoto hizo tumeshuhudia pia vyama vingi vya upinzani vikijitoa katika uchaguzi wa serikali za mitaa wa mwaka 2019. Miongoni mwa sababu za kujitoa zimeelezwa kuwa ni kutoridhishwa na mchakato wa kuweka wagombea kutoka vyama mbalimbali.

Board of Directors:
Ms. Vicky Ntetema, Michael  Kyande, Kenneth Simbaya, Deogratius Nsokolo, Maxence Melo, Christina Kamili, Jamila M. Juma, Hassan Kh. Juma, Edwin Soko.
*Defending Human Rights is not a Crime!*

**Wito Wetu**

i. Kwa kuzingatia changamoto zote zinazoathiri Watetezi wa Haki a Binadamu / AZAKI wakati wa uchaguzi; ni wakati muhimu sasa kwa Watetezi wa Haki za Binadamu / AZAKI kote nchini kutumia Kanuni za Maadili zilizozinduliwa na Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania ili kurudisha sifa njema ya Watetezi wa Haki za Binadamu / AZAKi.
ii. AZAKi ziendelee kuchukua hatua zinazofaa ili kuhakikisha kuwa masuala yote ya kimaadili yanayohitaji kufanyiwa kazi na Watetezi wa Haki za Binadamu / AZAKi yanashughulikiwa ipasavyo. Kanuni za Maadali ya Watetezi wa Haki za Binadamu katika uchaguzi zitakuwa mwongozo mzuri kwa Watetezi wa Haki za Binadamu wakati wote wa chaguzi na michakato mingine ya kidemokrasia.
iii. Tunaishauri wizara ya Ofisi ya Raisi Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ihakikishe kua inatoa vibali vya kutoa elimu ya uraia kwa wapiga kura na kuruhusu AZAKi kufanya uangalizi wa kwa mashirika yaliyoonyesha nia ya kufanya kazi hizo;
iv. Tunashauri wizara ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ihakikishe inachukua hatua stahiki kuhakikisha kua kasoro zote zilizojitokeza katika maandalizi ya uchaguzi huu wa serikali za mitaa zinaondolewa.
v. Tunaomba wizara ya Ofisi ya Raisi Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kuweka wazi takwimu kuhusu idadi ya AZAKI zilizoomba vibali vya kutoa elimu ya uraia na kuangalia uchaguzi ili umma wa watanzania wajue idadi kamili ya mashirika yaliyoomba, yaliyokubaliwa na yaliyokataliwa kujishughulisha na kazi hizo za uchaguzi.
vi. Asasi za Kiraia zilizopata vibali vya kutoa elimu ya uraia na kuangalia uchaguzi zihakikishe zinaendelea kufanya kazi hizo kwa weledi mkubwa ili kuweza kuhakikisha uchaguzi huo unafanyika kwa mujibu wa Katiba na sheria za Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania.
vii. AZAKI zilizoonesha nia ya kuangalia uchaguzi na kutoa elimu ya uraia kwa wapiga kura ziendelee kufuatilia majibu ya maombi yao katika wizara husika ili wizara iweze kutoa majibu
viii. Tunaingia kwenye uchaguzi wakati vyama vingi vimejiondoa kwenye mchakato wa uchaguzi, hivyo sisi wana Azaki na watetezi wa haki za binadamu tunatoa wito kwa serikali kuwa na kamati ya usuluhishi kati ya vyama vilivyotangaza kujitoa, viongozi wa dini na serikali.

**Imetolewa leo Tarehe 16 Novemba, 2019**
**Na**
**Wanachama wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania**

Board of Directors:
Ms. Vicky Ntetema, Michael Kyande, Kenneth Simbaya, Deogratius Nsokolo, Maxence Melo, Christina Kamili, Jamila M. Juma, Hassan Kh. Juma, Edwin Soko.
*Defending Human Rights is not a Crime!*

Tanzania Human Rights Defenders Coalition
[THRDC]
P. O. Box 105926 Dar es Salaam, Tanzania
Mob: +255 769 642 208 E-mail; info@thrdc.or.tz
Website: www.thrdc.or.tz

Board of Directors:
Ms. Vicky Ntetema, Michael Kyande, Kenneth Simbaya, Deogratius Nsokolo, Maxence Melo, Christina Kamili, Jamila M. Juma, Hassan Kh. Juma, Edwin Soko.